

Nyongeza ya Chanjo ya UVIKO-19

Dozi ya nyongeza ya chanjo ya UVIKO-19 ni nini?

Nyongeza ni dozi nyingine ya chanjo ya UVIKO-19. Unaweza kupata chanjo ya nyongeza miezi sita baada ya dozi mbili za kwanza. Maafisa wa afya ya umma wanapendekeza nyongeza ya pili kwa watu wenye umri wa miaka 50 na zaidi na wale ambao wana kinga dhaifu mwilini. Unaweza kupata maelezo zaidi hapa <https://www.nshealth.ca/coronavirusvaccine>

Kwa nini ninahitaji dozi ya nyongeza?

Baada ya chanjo ya awali, kinga yako hupungua baada ya muda, kwa hivyo bado unaweza kupata UVIKO-19. Nyongeza hufanya mfumo wako wa kinga kuwa imara dhidi ya UVIKO-19 kwa muda mrefu. Utajilinda wewe mwenyewe na watu wanaokuzunguka kwa kupata nyongeza.

Je, dozi za nyongeza za chanjo ni sawa na dozi mbili za kwanza?

Ndiyo. Chanjo za nyongeza za UVIKO-19 ni muundo sawa na chanjo za sasa za UVIKO-19. Lakini, nyongeza ya chanjo ya UVIKO-19 ya Moderna ni nusu ya dozi ambayo watu wallipata kwenye mfululizo wao wa awali

Je, "nimechanjwa kikamilifu" ikiwa sitapata dozi ya nyongeza?

Ndiyo. Kwa Pfizer na Moderna, umechanjwa kikamilifu wiki mbili baada ya dozi yako ya pili. Kwa Janssen, umechanjwa kikamilifu wiki mbili baada ya chanjo.

Ni nyongeza gani ninapaswa kupata?

1. Watu wa miaka 30 na zaidi wanaweza kupata dozi kamili ya Pfizer au nusu ya dozi ya Moderna. Haijalishi ulipata chanjo gani mwanzoni.
2. Wazee wanaoishi katika sehemu za Utunzaji wa Muda Mrefu wanahitaji dozi kamili ya Pfizer au kipimo kamili cha Moderna.
3. Watu miaka 18-29 wanapaswa kupata chanjo ya Pfizer kama nyongeza. Kuna hatari ndogo ya athari adimu kwenye moyo wako.
4. Watoto miaka 12-17 wenye matatizo ya kiafya ambayo ynaongeza hatari kwao ya ugonjwa mkali pia wanapaswa kupata dozi ya nyongeza ya Pfizer.

Ni kipindi gani cha kusubiri kupata chanjo kwa wale ambao wamepimwa na kukutwa na UVIKO-19?

Kwa taarifa zaidi kuhusu mkakati wa chanjo wa Nova Scotia, tafadhali tembelea: <https://novascotia.ca/coronavirus/vaccine/>.

Je, mwanamke mjamzito anaweza kupata nyongeza? Je, ni salama kwa mtoto mchanga?

Ndiyo, ni salama kwa mjamzito kupata chanjo, ikiwa ni pamoja na dozi za nyongeza. Wanawake wajawazito wana hatari ya kupata ugonjwa mbaya zaidi ikiwa wataambukizwa UVIKO-19, na chanjo zinasaidia kuzuia hili. Chanjo za UVIKO-19 hazina madhara kwa mtoto tumboni/mtoto mchanga. Aidha, kingamwili kutoka kwa mama hupitishwa kwa mtoto anaye endelea kukua tumboni, hivyo mtoto wao ana kinga fulani anapozaliwa. Mama pia anaweza kupitisha kingamwili kupitia maziwa yake ambayo pia yanaweza kusaidia kumlinda mtoto wake. Mama aliyechanjwa ana uwezekano mdogo wa kupitisha ugonjwa huo kwa mtoto wake. Mwanamke mjamzito anaweza kupata dozi ya kwanza ya nyongeza ya chanjo ya UVIKO-19 siku 120 baada ya dozi ya pili (au baada ya dozi 1 ya Janssen)

Je, nitahitaji nyongeza kila mwaka?

Bado haijafahamika ni kwa muda gani chanjo hizo zitatoa kinga na iwapo nyongeza inahitajika kila mwaka kama chanjo ya mafua. Kwa watu wazima, maswali haya ni muhimu sana kwa sababu kinga zetu hudhoofika tunapozeeka. Wataalamu wanachunguza mwingitio wa kinga ya muda mrefu kwa chanjo.

Je, ninaweza kupata UVIKO-19 ikiwa nilipata hapo awali?

Ndiyo, unaweza kupata UVIKO-19 ikiwa umekuwa nao hapo awali, haswa na Omicron. Chanjo inakupa kinga zaidi, hata kama tayari ulikuwa na UVIKO. Chanjo inaweza kusaidia kuzuia ugonjwa mkali na kifo hata kama utaambukizwa tena.

Vikwazo vingi sasa vimeondolewa. Je, hiyo inamaanisha kuwa UVIKO-19 haupo, au sio hatari tena?

Hapana, UVIKO-19 bado upo. Bado ni hatari kwa wazee na watu wenye magonjwa sugu, hasa ikiwa hawajachanjwa. Pia bado ni muhimu kufuata miongozo ya afya kama kuvaa barakoa sehemu za ndani, kunawa mikono mara kwa mara, kufunika mdomo wako unapokohoa, na kupata chanjo.

Lini ninaweza kupata nyongeza zangu za msingi?

Kuna tofauti kati ya dozi za chanjo na nyongeza, kulingana na umri, hali ya afya, na vigezo vya kustahiki:

Kati ya dozi ya pili na nyongeza ya kwanza:

- Siku 168 (wiki 24) kwa watu wenye umri wa miaka 12 - 69
- Siku 120 (wiki 17) kwa watu wenye umri wa miaka 70 na zaidi

Kati ya nyongeza ya kwanza na ya pili:

- Siku 168 (wiki 24) - Umri wa miaka 50 - 69
- Siku 120 (wiki 17) – Wajawazito waliopata nyongeza kabla ya kupata ujauzito.
- Siku 120 (wiki 17) - Watu wenye umri wa miaka 50 - 69 ambao wana kinga dhaifu kwa wastani mpaka dhaifu sana, na makundi yanayostahiki * (tazama hapa chini)

Tafadhali kumbuka: Afya ya Umma inapendekeza kupata nyongeza ya pili katika msimu wa "fall" kwa ulinzi bora wakati wa msimu ujao wa baridi na mafua. Pia, chanjo mpya ambazo zinaweza kutoa ulinzi mpana dhidi ya lahaja ya Omicron zinaweza kupatikana. Kwa habari zaidi, tafadhali angalia [hapa](#)

Ninawezaje kupata nyongeza?

Kabla ya kuanza:

- Unahitaji kadi halali ya afya ya Nova Scotia ili kuweka miadi mtandaoni.
- Unahitaji namba ya simu ikiwa italazimu kuwasiliana na wewe.
- Toa barua pepe unapoweka miadi yako. Utapokea barua pepe ya uthibitisho wa miadi yako, barua pepe ya kukumbusha siku moja kabla ya miadi yako, na barua pepe iliyo na rekodi yako ya chanjo baada ya miadi yako.

Jinsi ya kuomba miadi:

Unaweza kuomba miadi:

1. Mtandaoni kwa kliniki: <https://novascotia.flow.canimmunize.ca/en/covid-flu-booking>
2. Piga simu 1-833-797-7772 (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 1 asubuhi hadi saa 1 jioni na Jumamosi hadi Jumapili, saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni). Unahitaji kupiga simu kutoka kwenye nambari ya simu ya Canada na kuwa Canada unapopiga simu. Ikiwa mteja anahitaji ukalimani, hii ndiyo njia bora ya kuweka miadi (angalia "Huduma za Ukalimani zinazopatikana" hapa chini)

Kwa taarifa zaidi, angalia ISANS's [Jinsi ya Kuweka Miadi ya Chanjo - Tovuti ya mradi wa Beacon](#).

Jinsi ya kupata Kliniki ya Bila Miadi

Chanjo pia hutolewa katika kliniki mbalimbali za bila miadi. Maeneo na nyakati hizi hubadilika wiki hadi wiki. Unaweza kupata orodha mpya zaidi ya kliniki za jamii hapa: <https://www.nshealth.ca/drop-in-vaccine-clinics>.

Maduka ya dawa pia hutoa kliniki za bila miadi: <https://pans.ns.ca/walk-covid-19-vaccine-clinics>

Huduma za Ukalimani Zilizopo

Ikiwa unahitaji huduma katika lugha nyingine isipokuwa Kiingereza, unaweza kuomba mkalimani wakati unaomba miadi yako kwa simu 1-833-797-7772 (zaidi ya lugha 125 tofauti zinapatikana). Mtaalamu atapatia maswali yote ya afya na uchunguzi na wateja na kujibu wasiwasi na kusita kokote waliko nako wateja kuhusu chanjo.

Maduka ya dawa pia hutoa vipeperushi kwa lugha tofauti ambavyo wateja wanaweza kusoma wanapopata chanjo zao. Kunaweza pia kuwa na wafanyakazi sehemu hizo ambao wanaweza kukalimani.

Coronavirus (UVIKO-19)

Chanjo ya UVIKO-19

Vipindi vilivyopendekezwa kati ya dozi za chanjo

Usalama wa chanjo na madhara yanayowezezana

Chanjo ya UVIKO-19: Mwongozo wa Chanjo wa Canada

Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Chanjo ya UVIKO-19 | CDC